

Mapishi ya Ugali - Mtamu :-)

LENGO/MATOKEO:

Kupika Ugali kwa ajili ya watu 4-5

VIUNGO:

- Unga wa mahindi
- Maji
- Chumvi

MAELEKEZO/HATUA:

- 1 Weka maji kwenye sufuria kubwa, nzito. Ongeza chumvi kidogo. Acha mchanganyiko huo utokote, kisha uchote takribani kikombe kimoja cha mchanganyiko huo na uweke kando.
- 2 Weka unga polepole huku ukikoroga hadi umalize kuweka kiasi hicho chote kwenye sufuria, kidogo kidogo na uendelee kukoroga kwa mwiko ili kusiwe na mabonge yoyote. Pengine utahitaji kuondoa sufuria kwenye moto unapojaribu kuondoa mabonge ili kuzuia mchanganyiko huo usiungue.
- 3 Punguza kiwango cha joto hadi kiasi cha chini na upike mchanganyiko huo hadi uwe mzito.
- 4 Kisha weka maji yaliyotokota yaliyobaki, punguza joto, funika, kisha uache mchanganyiko huo uive kwa dakika kadhaa. Unaweza kuongeza maji, ukipenda. Zima moto. Pakua vidonge kwa bakuli dogo — tingisha na utengeneze kidonge kwa kulizungusha bakuli.
- 5 Chakula sasa kiko tayari kupewa walaji!

Chanzo: Maudhui haya yanahifadhiwa na Meta na hivi sasa yanajumuisha mafunzo yaliyotolewa kwa shirika la Youth and Media katika Kituo cha Berkman Klein cha Intaneti na Jamii katika Chuo Kikuu cha Harvard chini ya leseni ya Kimataifa ya Creative Commons Attribution-ShareAlike 4.0. Unaweza kuyatumia maudhui hayo, ikiwa ni pamoja na kuyanakili na kuandaa kazi zinazotokana na maudhui hayo, kwa madhumuni ya kibiashara au la, ilimradi utataja mradi wa Youth and Media kama chanzo cha asili na kufuata masharti mengine ya leseni hiyo, kushirikisha kazi zingine zozote za ziada chini ya masharti hayo.